

# Zab 67 - Atukuzwe Bwana

**Siku ya Mungu ya 22 katika mwaka C wa liturjia**

Eugène AMPIRE Bisimwa




1. Watu wema watafurahi, watashangilia,
   Mbele ya Mungu watachangamka kwa sherehe.
   MwimbieniMungu,lisifunijinalake:
   Jina lake ni Bwana, shangilieni mbele yake.

2. Baba wa yatima na mkinga wajane,
   Ndiye Mungu katika makao yake matakatifu.
   Mungu anawapatia walioachiliwa nyumba,
   Anawaondosha waliofungwa, anawapa uhuru.

3. Ulinyesha mvua ya mema, ee Mungu;
   Urisi wako uliporegea, Wewe uliutia nguvu:
   Ndipo watu wa ukoo wako wanapokaa,
   Ndipo mahali ulipomtengenezea mnyonge, kwa njia ya mema yako, ewe Mungu.